**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 03 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka 2021/2022.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

207. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika tukio muhimu zuri la kihistoria kwa nchi ya Zanzibar ni kufanyika kwa mkutano mkubwa wa tatu wa wana "Diaspora" mwishoni mwa mwezi wa Agosti, 2016 na kufunguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Saba.

(a) Baada ya kukamilika kwa Sera ya "Diaspora", Je, kuna mambo gani mazuri yaliyopatikana na kutekelezwa hadi sasa.

(b) Kwa kuwa wana "Diaspora" wanahitaji kuwa na kiunganishi, Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwaunganisha wana "Diaspora".

(c) Kwa kuwa Serikali ilichukuwa jitihada nzuri za kuwatambua wana "Diaspora" kote duniani, Je, Serikali imeshawatambua wana "Diaspora" wangapi na kukaa nao kwa ajili ya kuwaeleza azma ya Serikali.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

85. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha huduma za afya katika Kituo cha Afya Junguni ambacho kinasaidia sana kutoa huduma za afya kutokana na kuwepo kwa vifaa tiba vya kisasa na dawa za uhakika, hali inayopelekea wananchi wetu kuzidi kujenga imani kwa viongozi wao huku ikifahamika kwamba huduma za afya ni muhimu katika maisha ya jamii.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba kituo hiki mpaka kufikia mwezi wa Machi, 2021 kilikuwa na daktari mmoja tu ambaye anahudumia wakaazi wa Shehia zote tatu zinazotegemea kituo hiki.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka madaktari ambao wataongeza kasi ya kutoa huduma za afya katika kituo hiki.

(c) Je, Serikali haioni kama kuwepo kwa majengo na vifaa vya kutosha katika kituo hiki bila ya madaktari wa kutosha ni kutumia vibaya rasilimali za nchi.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

44. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya makampuni na taasisi binafsi ambazo zinaajiri wafanyakazi hapa Zanzibar zinaficha mishahara halisi ya wafanyakazi wao ili kukwepa kulipa kodi ya "PAYE" , hali inayopelekea Serikali kukosa mapato na kukwamisha juhudi za Serikali za kuwaletea maendeleo ya haraka wananchi wake.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na changamoto hii.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kinachokusanywa kwa mwezi kutoka kwa wafanyakazi wa sekta binafsi hapa Zanzibar.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

210. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali kwa nia njema imeanzisha Baraza la Vijana ili kusogeza ajira kwa vijana sambamba na kuwaunganisha katika kufanya miradi mbali mbali ya kuwasaidia kiuchumi.

(a) Je, hadi sasa Baraza hilo limetoa ajira ngapi kwa vijana wa Unguja na Pemba..

(b) Je, ni asilimia ngapi ya vijana wako kwenye vituo vya ujasiriamali na kuweza kujifunza kupitia mabaraza ya vijana.

(c) Je, ni asilimia ngapi ya vijana walengwa wanaonesha utayari wa kuyapokea mabaraza hayo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

151. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MANDOBA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Wakulima wengi wamehamasika kulima mazao ya mboga mboga na matunda lakini wakati wa mavuno soko linakuwa chini na kupelekea hasara kwa mkulima ambae alitumia mbegu, mbolea na huduma nyengine kwa ujumla.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wanawapatia masoko wakulima hawa wadogo wadogo.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

141. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika jitihada za kupunguza vifo vya mama na mtoto nchini, Serikali hukabiliana na changamoto hiyo kwa kuwasogezea akina mama huduma muhimu za afya karibu na makaazi yao.

Je, ni lini Serikali itaanzisha huduma za afya kumfikia mgonjwa (mobile doctors and clinics) katika maeneo yasiyofikika kirahisi (outreach areas).

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

197. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Miongoni mwa kero zinazowakabili walimu na wanafunzi wengi wanaosomea uwalimu hapa Zanzibar ni pamoja na kuondoshwa kwa mafunzo ya cheti cha ualimu katika chuo cha Nkuruma.

(a) Je, kuna mpango gani wa kurudisha mafunzo ya cheti cha ualimu katika chuo cha Nkuruma hasa

ikizingatiwa kuwa chuo hicho kilikuwa cha mwanzo kutowa mafunzo hayo.

(b) Je, mafunzo hayo yatarudishwa lini kwa manufaa na faida ya visiwa vyetu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

27. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Daraja la Chamanagwe linalounganisha miji ya Kusini na Kaskazini Pemba ni dogo, la zamani na lisilopitika. Siku za mvua kubwa za masika, maji hufunika daraja hilo na hali hii inapelekea usafiri na usafirishaji kushindikana kwa muda wa masaa au siku kadhaa katika kipindi chote cha mvua za masika.

Je, ni lini Serikali itajenga daraja la kisasa, kubwa na lenye kiwango ili kuondosha usumbufu katika eneo hilo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

115. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Kutokana na transfoma iliyopo maeneo ya Fuoni Kiembeni kuharibika mara kwa mara inaipelekea huduma ya umeme katika maeneo hayo kukosekana.

(a) Je, nini tatizo la transfoma hiyo.

(b) Je, Shirika lina mpango gani wa kuibadilisha transfoma hiyo ili wananchi wapate huduma ya umeme wa uhakika.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi
kwa Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**03 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**